# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU












# SERA YA TAIFA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2024

MACHI 2024

# SERA YA TAIFA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2024

**MACHI, 2024**

## YALIYOMO

VIFUPISHO .......................................................... vi

TAFSIRI YA DHANA/ UFAFANUZI WA ISTILAHI......... viii

DIBAJI ..........................................................x

**SURA YA KWANZA .............................................1**

1.1 Utangulizi..........................................................1

1.2 Hali Ilivyo..........................................................3

1.2.1 Uzalishaji wa Dawa za Kulevya ........................3

1.2.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya ..........................4

1.2.3 Udhibiti wa Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya ..........................................................6

1.2.4 Changamoto za Udhibiti wa Dawa za Kulevya ..........................................................13

**SURA YA PILI..........................................................16**

2.1 Umuhimu wa Sera..........................................16

2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera ....................18

2.2.1 Dira...........................................................18

2.2.2 Dhima........................................................18

2.2.3 Malengo ya Sera ........................................18

**SURA YA TATU........................................................19**

3.1 Uzalishaji na Utengenezaji wa Dawa za Kulevya ........................................................19

3.2 Usafirishaji, Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya....................................................20

3.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya .......................21

3.4 Uraibu na Magonjwa Yasiyoambukiza na Yanayoambukiza...........................................22

3.5 Uratibu wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya....................................................24

3.6 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika Kukabiliana na Tatizo la Dawa za Kulevya ........................................................25

3.7 Masuala Mtambuka........................................26

3.7.1 VVU na UKIMWI ...........................................26

3.8 Mazingira.......................................................26

**SURA YA NNE.........................................................28**

4.1 Mfumo wa Kisheria........................................28

**SURA YA TANO .......................................................30**

5.1 Muundo wa Kitaasisi ....................................30

5.1.1 Wizara yenye dhamana ya udhibiti wa Dawa za Kulevya ........................................................30

5.1.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya...................................................30

5.1.3 Wizara na Taasisi za Serikali .........................31

5.1.3.1 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa............................................31

5.1.3.2 Wizara yenye dhamana ya Kazi, Ajira na Vijana ..............................................................32

5.1.3.3 Wizara yenye dhamana ya Afya ....................32

5.1.3.4 Wizara yenye dhamana ya Maliasili na Utalii .33

5.1.3.5 Wizara yenye Dhamana na Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Makundi Maalum..33

5.1.3.6 Wizara yenye dhamana ya Elimu...................33

5.1.3.7 Wizara yenye dhamana ya Fedha .................34

5.1.3.8 Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi.............34

5.1.3.9 Wizara yenye dhamana ya Kilimo..................35

5.1.3.10 Wizara yenye dhamana na Mawasiliano........35

5.1.3.11 Wizara yenye dhamana ya Sheria .................35

5.1.3.12 Wizara yenye dhamana ya Viwanda na Biashara ........................................................35

5.1.3.13 Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa................................36

5.1.3.14 Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi ...............................................................36

5.1.3.15 Wizara yenye dhamana ya Madini .................36

5.1.3.16 Wizara yenye dhamana ya Nishati.................36

5.1.3.17 Wizara yenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi .36

5.1.3.18 Wizara yenye dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ...................................................37

5.1.3.19 Wizara yenye dhamana ya Mipango na Uwekezaji.....................................................37

5.1.3.20 Wizara yenye dhamana ya Mazingira ...........37

5.1.3.21 Wizara yenye dhamana ya Maji ....................37

5.1.3.22 Wizara yenye dhamana ya Ardhi na Makazi .37

5.1.3.23 Wizara yenye dhamana ya Ulinzi ..................37

5.1.3.24 Wizara yenye dhamana ya Utumishi.............38

5.1.3.25 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.........38

5.1.3.26 Vyombo vya Ulinzi na Usalama .....................38

5.1.3.27 Taasisi yenye dhamana ya Dawa na Vifaa Tiba ....................................................................38

5.1.3.28 Taasisi yenye dhamana ya Usimamizi wa Kemikali........................................................38

5.1.3.29 Tawala za Mikoa ..........................................39

5.1.3.30 Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji ....................................................................39

5.1.3.31 Ngazi ya Kata................................................39

5.1.3.32 Ngazi ya Kijiji/Mtaa........................................40

5.1.3.33 Ngazi ya Kaya ...............................................40

5.1.3.34 Sekta Binafsi .................................................40

5.1.3.35 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ..........41

5.1.3.36 Taasisi za Kidini ............................................41

5.1.3.37 Wadau wa Maendeleo ..................................41

5.1.3.38 Vyombo vya Habari.......................................41

5.2 Ufuatiliaji na Tathmini....................................42

5.3 Hitimisho .......................................................42

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CYCs | Taasisi ya Malezi ya Watoto na Vijana |
| HBV | Virusi vya Homa ya Ini aina B |
| HCV | Virusi vya Homa ya Ini aina C |
| INCB | Bodi ya Kimataifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya |
| MAT | Vituo vya Huduma za Matibabu kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| NPS | Dawa Mpya za Kulevya |
| NSP | Programu ya ugawaji wa mabomba na sindano kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga |
| RYCs | Huduma ya Makazi kwa Vijana |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika |
| TASAC | Shirika la Uwakala wa Huduma za Meli |
| TB | Ugonjwa wa Kifua Kikuu |
| THC | Kemikali za Kulevya katika Mmea wa Bangi |
| TMDA | Mamlaka ya Vifaa Tiba na Dawa |

| | |
|---|---|
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UNGASS | Mkutano Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya wa mwaka 2016 |
| UNODC | Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulika na Dawa za Kulevya na Uhalifu |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI |
| ZEP | Programu ya elimu kwa watoto wanaoishi kwenye familia za kipato cha chini |

## TAFSIRI YA DHANA/ UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Dawa za Kulevya** | Dawa za kulevya ni kemikali ambazo mtu akizitumia huathiri mfumo wa fahamu na kusababisha mabadiliko katika hisia, fikra na tabia. |
| **Huduma za utengemao** | Huduma za tiba na unasihi kwa waathirika wa dawa za kulevya |
| **Kemikali bashirifu** | Kemikali zinazoweza kuchepushwa kutoka kwenye matumizi halali na kutumika kutengeneza dawa za kulevya |
| **Kupunguza uhitaji** | Shughuli zote zinazolenga kupunguza matumizi ya dawa za kulevya |
| **Kupunguza madhara** | Shughuli zote zinazolenga kupunguza athari zinazosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya |
| **Kupunguza upatikanaji** | Shughuli zote zinazolenga kupunguza uingizaji, uzalishaji, utengenezaji na usambazaji wa dawa za kulevya |
| **Maabara bubu** | Maabara zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya kinyume cha sheria |
| **Mimea haramu** | Mimea ambayo inaweza kutumika kama dawa za kulevya au kuzalisha dawa za kulevya kinyume cha sheria. |

| | |
|---|---|
| **Uchepushwaji** | Kubadili matumizi halali ya kemikali bashirifu kutengeneza dawa za kulevya au kubadili matumizi halali ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama dawa za kulevya |
| **Utegemezi** | Uhitaji wa lazima wa dawa za kulevya licha ya madhara yake |
| **Waraibu** | Wategemezi wa matumizi ya dawa za kulevya |

# DIBAJI

Biashara na matumizi ya dawa za kulevya ni tatizo linaloathiri nchi nyingi duniani. Dawa za kulevya zina athari katika nyanja za afya, uchumi, siasa, mazingira, diplomasia, jamiiųsalama wa nchi na dunia kwa ujumla. Serikali imeazimia kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kwa kutunga sera ili kutoa mwongozo wa kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanakusudia kuiwezesha nchi kufikia malengo ya Kitaifa ya kudumisha amani, usalama na umoja; kuimarisha misingi ya utawala bora; kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine na kuimarisha ustawi wa jamii i.

Dira ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024 inalenga kuwa na jamii isiyojihusisha na uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Sera inaweka mkazo katika kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya; kudhibiti uhitaji wa dawa za kulevya; kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za tiba na utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya; na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine kupitia utekelezaji wa Itifaki na Mikataba mbalimbali.

Msisitizo wa sera ni kuweka uwajibikaji wa wadau katika udhibiti wa dawa za kulevya; kuimarisha tafiti kuhusu dawa za kulevya; kuimarisha doria na operesheni za mara kwa mara; na kufanya kaguzi katika vituo vya forodha, vyombo vya usafiri, kampuni za usafirishaji vifurushi na kwenye kampuni zinazojihusisha na biashara za kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini. Vilevile, Serikali itaendelea kuratibu na kupanua huduma za upataji nafuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya katika nyumba za upataji nafuu nchini.

Elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya itaendelea kutolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, semina, makongamano, mitandao ya kijamii na vipeperushi kama mkakati muhimu wa kupunguza matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa makundi rika tofauti kulingana na mahitaji. Vilevile, Serikali itaendelea kushirikiana na mataifa mengine na taasisi za kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya ili kubadilishana uzoefu, kushiriki mafunzo na kupanga mikakati ya pamoja ya namna ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Ushirikiano huo utasaidia kupunguza uhalifu hasa katika ukanda wa bahari kuu ambako ndiyo njia kuu ya kupitishia dawa za kulevya na uhalifu mwingine wa kupangwa.

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanahitaji ushiriki wa wadau wote wakiwemo Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Kidini, Washirika wa Maendeleo na jamii nzima. Aidha, jitihada za pamoja zinahitajika kwa kuimarisha ushirikiano na nchi jirani ili kufikia azma ya kutatua tatizo la dawa za kulevya kwa lengo la kuboresha, ustawi wa maisha ya watu na kudumisha amani na usalama wa nchi.

Napenda kutoa shukrani kwa wataalam wa Wizara na wadau wengine waliochangia na kuwezesha kukamilika kwa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya

Mwaka 2024. Ofisi ya Waziri Mkuu itashirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sera hii inatekelezwa kwa maslahi ya Taifa na ustawi wa jamii hapa nchini.

Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)
**WAZIRI MKUU**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazokabiliwa na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Bangi ni dawa ya kulevya inayoongoza katika matumizi hapa nchini ikifuatiwa na mirungi, *heroin* na *cocaine*. Tatizo la bangi na mirungi limekuwepo kabla ya uingizwaji wa dawa za *heroin* kutoka Kusini - Mashariki mwa Bara la Asia hasa nchi za Afghanistan na Pakistani na *cocaine* kutoka Bara la Amerika ya Kusini hasa nchi za Colombia na Brazil. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu ya mwaka 2022, watumiaji wa dawa za kulevya duniani ni wastani wa watu milioni 284. Watumiaji wa bangi pekee walikuwa milioni 209, afyuni milioni 61, *amphetamine* milioni 34, cocaine milioni 21 na *ecstasy* milioni 20. Vilevile, dawa mpya za kulevya *(New Psychoactive Substance* - NPS*)* zaidi ya kemikali 1028 zilizotolewa taarifa na shirika la umoja wa Mataifa mwaka 2018 zimeanza kuingizwa na kutumika nchini.

Uingizwaji wa dawa za kulevya kwa wingi hapa nchini ulianza mwanzoni mwa miaka ya 1980. Hii ilitokana na uwepo wa migogoro iliyosababisha kuimarika kwa ulinzi katika nchi ambazo zilikuwa ni njia ya upitishaji wa dawa za kulevya kuelekea katika masoko ya Ulaya, Marekani na Australia. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kutumika kama njia mbadala ya usafirishaji wa dawa za kulevya kwenda kwenye masoko hayo. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017, nchi yetu ilianza kushuhudia wimbi la uingizaji na uchepushwaji wa kemikali bashirifu pamoja na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa Taarifa za Hali ya Dawa za Kulevya Nchini kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2012 hadi 2022, jumla ya tani 460.59 za bangi; tani 196.82 za mirungi, kilogramu 265.5 za *cocaine* na kilogramu 254.7 za heroin zilikamatwa. Vilevile, kilogramu 22,143 na lita 304,513 za kemikali bashirifu zilikamatwa na tani 603.1 zilizuiwa kuingia nchini. Kadhalika, kuanzia mwaka 2021 kumekuwa na ongezeko la uingizaji wa dawa za viwandani ikiwemo *methaphetamine*.

Katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari hadi Desemba 2023 jumla ya kilogramu 1,965,340.52 zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 10,522. Kiwango cha ukamataji uliofanyika mwaka 2023 cha kilogramu 1,965,340.52 ni kikubwa ikilinganishwa na kiasi cha kilogramu 660,465.4 kilichokamatwa kwa miaka 11 kuanzia mwaka 2012 hadi 2022.

Taarifa za Hali ya Dawa za Kulevya Nchini za mwaka 2020 na 2022 zinabainisha kuwa idadi ya waraibu wa dawa za kulevya na vilevi vingine imeongezeka kutoka 169,269 mwaka 2020 hadi 854,134 mwaka 2022 ambapo asilimia 78 ni vijana wenye umri kati ya miaka 15-35.

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini za mwaka 2020 na mwaka 2021 zinaonesha kuwepo kwa matumizi haramu ya dawa tiba zenye asili ya kulevya hususan *pethidine, fentanyl, kundi la dawa za benzodiazepine, codeine, barbiturate* na *tramadol*.

Msukumo wa kuwa na Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024 unatokana na upungufu wa mfumo uliopo kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambayo imejikita katika kushughulikia makosa ya kijinai na kuacha masuala ya kisera yakiwemo matamko kuhusu wajibu wa wadau katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya; tafiti

mbalimbali kuhusu dawa za kulevya; ushughulikiaji wa maadili ya jamii; huduma za tiba; malezi na utengamao; na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu madhara ya dawa za kulevya. Aidha, msukumo zaidi unatokana na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea duniani ya kijamii, kisayansi, kiteknolojia, kiafya, kimazingira na kiusalama. Vilevile, kutungwa kwa sera hii ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 245; Azimio la Bunge la mwaka 2022; na matakwa ya Itifaki na Mikataba ya kikanda na kimataifa yanayozitaka nchi wanachama kuwa na sera mahsusi ya kushughulikia tatizo la dawa za kulevya.

Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 inaweka misingi imara ya kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya nchini kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Vilevile, sera inaweka mifumo wezeshi ya utekelezaji wa miongozo, itifaki na mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

## 1.2 Hali Ilivyo

### 1.2.1 Uzalishaji wa Dawa za Kulevya

Katika miaka ya hivi karibuni, uzalishaji wa dawa za kulevya umeongezeka kutokana na matumizi ya njia za kisasa za uzalishaji ikiwemo matumizi ya mbegu za kisasa na mimea mseto, teknolojia ya kisasa pamoja na uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022 imebaini kuwepo kwa uzalishaji wa mimea aina ya bangi yenye kiwango cha kemikali aina ya *Tetrahydrocannabinol* (THC) mara nne zaidi ya bangi ya kawaida hivyo kuwa na madhara zaidi kwa mtumiaji. Dawa hii imeanza kutumika katika bidhaa za vyakula kama vile biskuti, keki, pipi na baadhi ya vinywaji mbalimbali.

Bangi inalimwa zaidi katika Mikoa ya Mara, Arusha, Morogoro, Iringa, Kilimanjaro, Mbeya, Tabora, na Rukwa. Katika mwaka 2012 hadi 2022 jumla ya tani 460.59 za bangi; tani 196.82 za mirungi; tani 2.789 za *heroin*, kilogramu 265.521 za *cocaine* na kilogramu 430.77 za dawa za kulevya aina ya *methaphetamine* zilikamatwa. Vilevile, kati ya mwaka 2017 hadi 2022, zaidi ya tani 600 na lita 304,513 za kemikali bashirifu zinazoweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya zilizuiliwa kuingia nchini kutokana na ukiukwaji wa taratibu za kuingiza bidhaa hizo nchini ikiwemo udanganyifu wa wamiliki halali wa bidhaa hizo.

Tathmini inaonesha mwaka 2018 aina ya dawa mpya 1,028 zilizalishwa kutokana na kemikali bashirifu. Dawa hizo zina kiwango kikubwa cha kulevya na hazipo kwenye orodha ya dawa zinazodhibitiwa kimataifa na hivyo hutengenezwa kwa lengo la kukwepa mikondo ya kisheria na kurahisisha usafirishaji. Utambuzi wa dawa hizo mpya umekuwa na changamoto kutokana na dawa hizo kutotambuliwa kirahisi na mifumo iliyopo ya udhibiti.

Aidha, udhibiti wa dawa hizo umekuwa na changamoto kutokana na kuwepo kwa mbinu mpya za usafirishaji wa dawa za kulevya zikihusisha nchi kavu, anga na majini; matumizi ya wanyama na ndege kama njiwa; matumizi ya ndege zisizo na rubani; masoko ya mitandao isiyo rasmi (*dark-web*); na vifurushi kupitia kampuni za kusafirisha vifurushi.

### 1.2.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2022 inaonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2020 zaidi ya watu milioni 284 duniani wanakadiriwa kutumia dawa za kulevya sawa na uwiano wa 1:18 ya watu wenye umri kati ya miaka 15 – 64. Aidha, idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya duniani inakadiriwa kuwa itaongezeka kwa asilimia 11 ifikapo

mwaka 2030 na zaidi ya asilimia 40 kwa Afrika pekee. Tafiti zinabainisha kuwa matumizi ya dawa za kulevya Kusini mwa Jangwa la Sahara yataongezeka kwa asilimia 5 kwa mwaka na kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2050.

Aidha,taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini ya mwaka 2021 inaonesha matumizi ya dawa za kulevya yapo zaidi katika maeneo ya majiji, miji mikuu ya Mikoa na kusambaa katika miji midogo hasa iliyopo kandokando ya barabara kuu ziendazo mikoani. Mikoa yenye matumizi makubwa ya dawa za kulevya ni Dar es Salaam, Tanga, Pwani,Mwanza, Arusha, Morogoro, Dodoma, Mara na Mbeya. Aidha, Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2022 inaonesha hadi kufikia Desemba 2022, waraibu 854,134 (wanaume wakiwa 434,847 (50.91%) na wanawake 419,287 (49.08%) walipata tiba za uraibu kwenye vitengo vya afya ya akili katika Hospitali za Wilaya, Mikoa, Kanda na Rufaa kutokana na matumizi ya vilevi na dawa mbalimbali za kulevya. Aidha, Huduma ya Tiba ya *Methadone* iliwafikia waraibu wa dawa za kulevya aina ya *herion* 13,696 (wanaume wakiwa 13,089 (95.56%) na wanawake 607 (4.44%) kupitia vituo 16 vilivyopo nchini.

Baadhi ya sababu zinazochangia watu kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ni pamoja na: upatikanaji kwa urahisi wa dawa za kulevya zinazotokana na mimea kama vile bangi na mirungi; msukumo wa makundi rika; jamii kutokuwa na uelewa sahihi kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kiafya; sababu za kijamii na kiuchumi; migogoro, na unyanyapaa. Aidha, utengano wa kifamilia umesababisha kukosekana kwa malezi bora kwa watoto na vijana hivyo baadhi yao kujiunga na makundi yanayotumia dawa za kulevya; magonjwa ya akili kama vilesaikosisi; msongo wa mawazo; sonona na kihoro; na ukuaji wa teknolojia, utandawazi na mitandao ya kijamii vimechangia kwenye mmomonyoko wa maadili kwa vijana kuiga maisha, mitindo, mila na desturi za kigeni ikiwemo kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

### 1.2.3 Udhibiti wa Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya

Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kudhibiti matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

**a) Mifumo ya Kisheria na Kitaasisi**

Serikali ilianzisha Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya ndani ya Jeshi la Polisi mwaka 1991, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya mwaka 1997 pamoja na kuandaa Mpango Kabambe wa Kudhibiti Dawa za Kulevya Mwaka 2002 hadi 2006 kwa lengo la kuratibu mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Aidha, mwaka 2015 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 ili kuweka msukumo wa utekelezaji wa afua za kudhibiti dawa za kulevya nchini. Sheria hiyo ilianzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yenye jukumu la kufafanua, kuhamasisha, kuratibu na kutekeleza hatua zote za udhibiti wa dawa za kulevya. Sheria hiyo imeainisha makosa na adhabu zinazopaswa kutolewa kwa wahusika wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Tathmini imebaini mfumo uliopo kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 una upungufu kwa kuwa umejikita katika kushughulikia makosa ya kijinai baada ya kudhihirika kwa vitendo vya biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo, mawanda mapana ya udhibiti wa dawa za kulevya yanapaswa kujikita katika hatua za kisera zinazopaswa kuchukuliwa kabla, wakati na baada ya kubainika kwa vitendo viovu vya dawa za kulevya. Masuala ya kisera ambayo hayashughulikiwi na sheria ni pamoja na kutobainishwa kwa wajibu wa sekta na wadau mbalimbali katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za

kulevya; tafiti mbalimbali kuhusu dawa za kulevya; huduma za kinga, tiba, matunzo na utengamao kwa waraibu; makosa dhidi ya maadili ya jamii; utoaji wa elimu kwa umma; na uchopekaji wa dhana ya udhibiti wa dawa za kulevya katika sera za kisekta.

Mifumo mingine ya kisheria inayotumika sambamba na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ni pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306; Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443; Sheria ya Miamala ya Kielekroniki, Sura ya 442; Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu,Sura 423; Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256; Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254; Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61; na  Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368. Utekelezaji wa Sheria hizo kwa kiasi kikubwa umesaidia kuimarisha udhibiti  wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kuvunja na kudhoofisha mitandao mikubwa ya biashara ya dawa za kulevya mfano, kukamatwa kwa wafanyabiashara wakubwa ambao pia, walikuwa wakitafutwa na nchi nyingine duniani. Pamoja na mafanikio hayo, sheria hizo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuimarisha mfumo wa udhibiti na kuweka msimamo wa nchi kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya. Masuala yanayohitaji kushughulikiwa na kudhibitiwa ni ongezeko la matumizi ya mitandao isiyo rasmi (darknet) na fedha za kidijitali ambayo haidhibitiwi na mifumo ya fedha iliyopo.

### b) Kuridhia na Kutekeleza Itifaki na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa

Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ikiwa ni pamojana kuridhia na kutekeleza Mikataba Mitatu (3) ya Kimataifa inayosimamiwa na Ofisi yaUmoja wa Mataifa inayoshughulika na Dawa za Kulevya na Uhalifu. Mikataba hiyo niMkataba wa Kudhibiti Dawa za Kulevya za Nakotiki wa mwaka 1961; Mkataba wa Kudhibiti Dawa za Saikotropiki, 1971; na Mkataba Dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Dawa za Nakotiki na Saikotropiki, 1988. Aidha, Tanzania inatekeleza Itifaki za kikanda katika udhibiti wa Dawa za Kulevya ikiwemo Itifaki ya Kupambana na Dawa za Kulevya Katika Nchi za Kusini mwa Afrika SADC, 1999; Itifaki ya Kupambana na Usafirishaji na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2001; na Mpango kazi wa Umoja wa Afrika wa Kudhibiti Dawa za Kulevya na Kuzuia Uhalifu 2019 - 2025.

Jitihada nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kutekeleza makubaliano ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2016 Kuhusu Majadiliano ya Kukabiliana na Tatizo la Dawa za Kulevya Duniani; utekelezaji wa tamko la Kisiasa la Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu la mwaka 2009 ambapo Kifungu cha 4(a) kinaelekeza nchi wanachama kutunga sera toshelevu za kudhibiti dawa za kulevya pamoja na makubaliano ya Mawaziri wa Nchi wanachama wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu ya mwaka 2019 kuhusiana na kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuridhia na kusaini mikataba ni pamoja na kuimarika kwa ushirikiano na uhusiano katika jitihada za kupambana na dawa za kulevya kwa kuhakikisha kunakuwepo na uelewa na msimamo wa pamoja; kubadilishana taarifa za kiintelijensia; na kubadilishana uzoefu na mbinu za kudhibiti dawa za kulevya. Itifaki na Mikataba hiyo inaelekeza nchi wanachama kuwa na sera

mahsusi za kushughulikia tatizo la dawa za kulevya.

Hata hivyo, Tanzania haina Sera inayotoa mwongozo, msimamo na mwelekeo wa nchi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambao ni muhimu katika kutoa msukumo wa utekelezaji wa mikataba na Itifaki ambazo nchi imeridhia. Itifaki na Mikataba hiyo imeelekeza nchi wanachama kutunga sera ili kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya. Vifungu vya 1 (m) na 7 (h) vya makubaliano ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2016 vinaitaka nchi kutunga sera toshelevu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ili kuimarisha udhibiti. Maelekezo hayo pia yametolewa kupitia Kifungu cha 4 (a) cha Mkataba wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu; na kifungu cha 7 cha Itifaki ya Kupambana na Biashara ya Dawa za Kulevya Eneo la Kusini mwa Bara la Afrika. Hivyo, kutungwa kwa sera hii ni utekelezaji wa makubaliano ya Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya kuimarisha juhudi za pamoja za kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya ambalo halina mipaka.

### c) Elimu kwa Umma kuhusu Madhara ya Dawa za Kulevya

Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya kupitia vyombo vya habari, makongamano, matukio na maadhimisho ya kitaifa. Aidha, Serikali imeendelea kujenga uelewa wa udhibiti wa dawa za kulevya kwa wadau mbalimbali zikiwemo taasisi za elimu, vyombo vya ulinzi na usalama, waendesha mashtaka, wapelelezi, na vyombo vya habari. Vilevile, Tanzania huadhimisha siku ya kupiga vita dawa za kulevya tarehe 26 Juni kila mwaka ambayo hutumika kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

Utoaji wa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya

unakabiliwa na changamoto ya mwitikio mdogo wa jamii kutokana na wadau wengine kutopewa nguvu kisera jukumu la kutoa elimu. Mfumo uliopo kupitia Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 hautoi wajibu kwa wadau kushiriki katika utoaji wa elimu. Aidha, mitaala ya elimu haijazingatia utoaji wa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya katika ngazi zote za elimu nchini.

### d) Utoaji wa Huduma kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya nchini kwa kuongeza na kuimarisha vituo vya utoaji huduma za tiba kwa waraibu; kuimarisha na kupanua huduma za nyumba za upataji nafuu; nakuimarisha vitengo vya afya ya akili katika hospitali za Mikoa.

Suala la utoaji huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya linakabiliwa na changamoto za kukosekana kwa utayari kwa waraibu wa dawa za kulevya kujitokeza kupata hudumakwa hofu ya kunyanyapaliwa na jamii, kufahamika, kuchukuliwa hatua pamoja na kutokuwa tayari kuacha matumizi ya dawa za kulevya; kukosekana kwa vituo vya kutosha vya utengamao na mafunzo ya amali (*Vocational Training Centers*) kwa waraibu waliopata nafuu; uwepo wa magonjwa mengine kama vile UKIMWI, magonjwa ya akili na magonjwa yasiyoambukiza; kukosekana kwa mahitaji na huduma muhimu kwenye nyumba za upataji nafuu; na idadi kubwa ya waraibu wa dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi, *heroin*, dawa tiba zenye asili ya kulevya na cocaine kuliko uwezo wa Serikali na Asasi za Kiraia hivyo kusababisha utoaji wa huduma isiyokidhi mahitaji.

Hata hivyo, mfumo uliopo wa kisheria hautambui majukumu ya utoaji wa huduma hizo kwa waraibu. Hivyo, sera imelenga

kutoa wajibu wa kuhudumia waraibu kwa kuwapatia huduma za tiba, malezi, matunzo na utengamao ili kuleta ustawi wa jamii hiyo. Aidha, sera inaweka mfumo wa kuwezesha waraibu waliopata nafuu kupatiwa ujuzi na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za kiuchumi na ajira.

### e) Operesheni za Dawa za Kulevya

Serikali imeendelea na jitihada za kudhibiti usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya nchini kwa kuimarisha doria katika ukanda wa bahari, viwanja vya ndege na vituo vya forodha vya mipakani. Aidha, Serikali imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali za kushtukiza kwenye maeneo yanayohisiwa kuendesha biashara za dawa za kulevya katika vyombo vya usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo, viwanda na makampuni yanayojishughulisha na kemikali na dawa tiba pamoja na kwenye mashamba yanayohisiwa kuwa na kilimo cha dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi. Vilevile, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya katika hospitali na vituo vingine vya kutolea huduma za afya.

Pamoja na jitihada hizo, changamoto ya kubadilika mara kwa mara kwa mbinu za usafirishaji wa dawa za kulevya kutokana na kukua kwa matumizi ya sayansi na teknolojia; ongezeko la uzalishaji wa dawa za kulevya kutoka nchi zalishi zikiwemo dawa mpya zinazotokana na kemikali bashirifu; ongezeko la watumiaji na wafanyabiashara wa dawa za kulevya; ukanda mrefu wa bahari na mipaka yenye vipenyo vingi hali inayosababisha ugumu katika kudhibiti wafanyabiashara wa dawa za kulevya; Tanzania kuwa kwenye eneo la kijiografia linalotumika kama njia ya kupitishia dawa za kulevya na kemikali bashirifu kuelekea maeneo mengine duniani; bei kubwa ya dawa za kulevya inayohamasisha watu wengi kutamani kujiingiza kwenye biashara hii haramu; na ushiriki mdogo wa jamii katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

## f) Ushirikiano na Wadau Wengine

Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ili kufikia malengo ya udhibiti wa dawa za kulevya nchini. Ushirikiano huo umejikita katika kuimarisha mifumo ya kubadilishana taarifa za kiintelijensia, kupata mafunzo ya kitaalamu, kubadilishana uzoefu na mbinu mbalimbali za udhibiti, kufanya operesheni za pamoja na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa uelewa kwa jamii juu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya; kuwa na mikakati ya pamoja kati ya nchi moja na nyingine katika udhibiti wa dawa za kulevya; kuongezeka kwa uwezo wa utambuzi na ukamataji wa dawa za kulevya na kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Hata hivyo, ushirikiano na wadau wengine unakabiliwa na changamoto ya mwitikio mdogo wa baadhi ya wadau katika kushiriki kikamilifu kwenye mapambano dhidi ya dawa ya kulevya nchini. Mwelekeo wa sera ni kuimarisha ushiriki wa wadau wa ndani na nje ya nchi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwenye hatua zote kabla, wakati na baada ya tatizo la dawa za kulevya kubainika.

## g) Masuala ya Maadili ya Jamii

Makosa dhidi ya maadili ya jamii yanawekwa kwenye kundi la makosa makubwa ya jinai. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi nchini, kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2014 hadi 2020 zinabainisha kuwa makosa ya dawa za kulevya yanachukua wastani wa asilimia 50 ya makosa yote yanayoathiri maadili ya jamii ikilinganishwa na makosa mengine. Aidha, Sheria ya

Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 haijatoa mwongozo wa kushughulikia masuala ya ukuzaji wa maadili ili kuiepusha jamii kujiingiza katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Sera imetoa wajibu kwa wadau kushiriki katika kukuza maadili ya jamii ili kuinusuru jamii dhidi ya madhara ya dawa za kulevya.

**h) Tafiti za Dawa za Kulevya**

Tafiti kuhusu utekelezaji wa afua za dawa za kulevya ni muhimu kwa ajili ya kuboresha sera, sheria, takwimu na utoaji maamuzi kuhusu kuimarisha mipango na mikakati ya kukabiliana na dawa za kulevya. Hata hivyo, mifumo ya kiutendaji iliyopo haijatoa jukumu kwa mamlaka na wadau kufanya tafiti mbalimbali za kisera na kisayansi kuhusu mwenendo wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini. Tafiti zinazogusa afua za dawa za kulevya zinahusisha wadau mbalimbali ambao kiutendaji hawaingiliani na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Miongoni mwa tafiti zinazotakiwa kufanyika ni kubaini aina mpya ya dawa za kulevya, idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya nchini, athari za dawa za kulevya kiafya, kijamii, kiuchumi na kimazingira. Kukosekana kwa mwongozo wa kisera kuhusu kufanyika kwa tafiti za afua za dawa za kulevya kunachangia kukosekana kwa takwimu muhimu kwa ajili ya kuboresha sera na mipango iliyopo ya udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

### 1.2.4 Changamoto za Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Udhibiti wa dawa za kulevya nchini unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a) Kuongezeka kwa waraibu wa dawa za kulevya kutoka 169,269 mwaka 2020 hadi 854,134 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 404 ambapo asilimia 78 ni

vijana wenye umri kati ya miaka 15-35. Tatizo la uraibu linachangia katika magonjwa ya afya ya akili kwa jamii; kuathiri nguvu kazi ya Taifa; kuongeza gharama kwa Serikali za kuwahudumia waraibu; na kuongezeka kwa idadi ya wategemezi katika jamii.

b) Kuendelea kuwepo kwa kiwango kikubwa cha uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya ambapo kati ya mwaka 2012 hadi 2022 kiasi cha tani 460.59 za bangi, tani 196.82 za mirungi na kilogramu 265.521 za *cocaine* kilikamatwa. Kukamatwa kwa kiwango kikubwa cha dawa za kulevya hapa nchini kunatokana na sababu za kijiografia zinazochangiwa na uwepo wa ukanda mrefu wa bahari; na hali ya hewa ya kitropiki inayoruhusu uzalishaji wa bangi na mirungi. Kiwango kikubwa cha upatikanaji wa dawa za kulevya hapa nchini kinaweza kuchangia ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya na kuathiri nguvukazi ya Taifa.

c) Kuwepo kwa kiwango cha dawa ya Heroin kilichokamatwa hapa nchini ambapo kilogramu 254.71 zilikamatwa mwaka 2022. Dawa hii inaweza kuleta madhara mbalimbali ikiwemo kuharibu mfumo wa fahamu; ugonjwa wa afya ya akili; kuleta uraibu; magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa shinikizo la damu, kisukari na na wakati mwengine kusababisha vifo;

d) Kuongezeka kwa matumizi ya kemikali bashirifu ambapo kati ya mwaka 2012 hadi 2023 jumla kilogramu 22,143 na lita 304,513 za kemikali bashirifu zilikamatwa na tani 603.1 zilizuiwa kuingia nchini;

e) Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kuwashirikisha wadau katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa

kulevya. Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka linalohitaji wadau mbalimbali katika kukabiliana nalo. Mifumo iliyopo ya udhibiti wa dawa za kulevya haijatoa wajibu kwa wadau mbalimbali kushiriki katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Hali hiyo inasababisha kukosekana kwa juhudi za pamoja za kukabiliana na tatizo hilo ambalo lina athari kwa jamii na Taifa kwa ujumla;

f) Kuongezeka kwa matumizi ya mitandao (dark-web) na fedha za kidijitali (cryptocurrency) yanayohusisha usafirishaji wa dawa za kulevya. Matumizi ya mitandao yanarahisisha upatikanaji wa taarifa pamoja na kuwezesha malipo kwa njia ya fedha za kidijitali pasipo kudhibitiwa na mamlaka za udhibiti wa masuala ya fedha na mawasiliano. Kuimarika kwa teknolojia hii kunachangia kukua kwa biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

g) Kukosekana kwa mifumo imara ya tafiti zinazolenga kudhibiti dawa za kulevya na athari zake kiuchumi, kijamii, kiafya na kimazingira. Kukosekana kwa tafiti kunachangia kutojulikana kwa ukubwa na athari za tatizo la dawa za kulevya. Aidha, tafiti zinaweza kusaidia kubaini aina mpya ya dawa za kulevya na kuiwezesha Serikali kuandaa mikakati mipya ya kukabiliana na dawa hizo.

# SURA YA PILI

# UMUHIMU WA SERA

## 2.1 Umuhimu wa Sera

Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuiathiri Tanzania hasa katika nyanja za kiuchumi, kiafya, kijamii, kisiasa, kimazingira pamoja na ulinzi na usalama wa nchi. Aidha, wafanyabiashara wa dawa za kulevya wameendelea kubuni mbinu mpya za uzalishaji na usafirishaji wa dawa za ikilinganisha na njia zilizotumika hapo awali. Uzalishaji kwa sasa umeongezeka na unatumia mbinu za kisayansi kama vile matumizi ya mbegu na mimea mseto, teknolojia ya kisasa pamoja na uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Mabadiliko haya ya kisayansi na teknolojia yameleta msukumo kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea kutunga sera ili kuimarisha mifumo ya udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Idadi kubwa ya watumiaji wa dawa za kulevya ni vijana kwa wastani wa asilimia 78. Hivyo, dawa za kulevya zinaathiri nguvu kazi ya Taifa ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Sera ya Taifa ya dawa za kulevya inakusudia kuweka mfumo wa kisera kwa ajili ya kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya katika nyanja za kupunguza uhitaji, kupunguza upatikanaji, kupunguza madhara na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Msukumo wa kutunga Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 unatokana na upungufu wa mfumo uliopo kupitia Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambayo imejikita katika kushughulikia makosa ya kijinai baada ya kubainika kwa tatizo la dawa za kulevya. Mfumo huo haujaweka misingi ya utekelezaji wa masuala ya kisera

ambayo yana mchango mkubwa katika kuiepusha jamii kujiingiza katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, kutungwa kwa sera hii ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2020 – 2025 Ibara ya 245 (a)-(e) ambayo imeielekeza Serikali kuchukua hatua za kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa kuimarisha mifumo ya udhibiti; azimio namba 3.4 (a) la Bunge lililotolewa Februari 2023 linaloelekeza Serikali kukamilisha mchakato wa kutunga Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024. Vilevile, mabadiliko yaliyotokea kitaifa, kikanda na kimataifa yametoa msukumo kwa nchi wanachama kutunga sera mahsusi ya kushughulikia tatizo la dawa za kulevya. Makubaliano hayo ni pamoja na Itifaki ya Kupambana na Dawa za Kulevya katika Jumuiya ya Kusini mwa Afrika ya mwaka 1999 katika Ibara ya 7; Ibara ya 7 ya mkataba wa Afrika Mashariki; Mpango Kazi wa utekelezaji wa Umoja wa Afrika kuhusu Udhibiti wa Dawa za Kulevya 2019 – 2025 na makubaliano ya Kikao Maalum cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Matifa wa mwaka 2016 katika Ibara ya 7 (h) na 1 (m). Aidha, mabadiliko ya kiuchumi, kimazingira, kijamii na kiteknolojia yameongeza matumizi ya mitandao (dark-web) na fedha za kidijitali (cryptocurrency) katika kuchochea usafirishaji wa dawa za kulevya na matumizi ya kemikali bashirifu katika kutengeneza dawa za kulevya.

Uwepo wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 utawezesha nchi kuwa na mfumo imara wa kudhibiti dawa za kulevya kwa kushirikiana na nchi nyingine ili kuifanya jamii na dunia kuwa salama katika kuchochea maendeleo na ustawi wa watu.

## 2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera

### 2.2.1 Dira

Kuwa na jamii isiyojihusisha na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

### 2.2.2 Dhima

Kudhibiti na kupambana na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa ustawi wa Taifa.

### 2.2.3 Malengo ya Sera

#### 2.2.3.1 Lengo la Jumla

Kuimarika kwa uwezo wa nchi katika kudhibiti na kupambana na biashara na matumizi ya dawa zakulevya.

#### 2.2.3.2 Malengo Mahsusi

a) Kudhibiti uzalishaji na utengenezaji wa dawa za kulevya;

b) Kudhibiti uingizwaji, usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini;

c) Kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini;

d) Kupunguza uraibu wa dawa za kulevya, magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza kutokana na matumizi ya dawa za kulevya;

e) Kuimarisha uratibu wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini; na

f) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya.

# SURA YA TATU

## HOJA NA MATAMKO YA SERA

### 3.1 Uzalishaji na Utengenezaji wa Dawa za Kulevya

Tanzania ni nchi ya kitropiki inayowezesha ustawi wa mimea aina ya bangi na mirungi ambayo inatokana na uoto wa asili. Uwepo wa uhitaji wa dawa za kulevya zinazotokana na mimea hiyo unachangia ongezeko la uzalishaji wake. Aidha, kiwango kikubwa cha kemikali bashirifu zinazokamatwa kinaashiria uwezekano wa dawa za kulevya kutengenezwa hapa nchini.

Serikali imeendelea kuweka juhudi katika mapambano dhidi ya uzalishaji na utengenezaji wa dawa haramu. Hata hivyo, tatizo la uzalishaji wa dawa zinazotokana na mimea bado ni kubwa. Athari za uzalishaji na utengenezaji wa dawa za kulevya huchangia kuongezeka kwa usambazaji wa dawa hizo na kuathiri afya ya jamii na nguvu kazi, uchumi wa nchi, kuongezeka kwa vitendo vya kihalifu na kuhatarisha usalama wa nchi.

#### 3.1.1 Lengo

Kudhibiti uzalishaji na utengenezaji wa dawa za kulevya

#### 3.1.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

a) *Itaimarisha udhibiti wa kilimo cha mimea yenye asili ya dawa za kulevya;*

b) *Itaboresha mifumo ya udhibiti, kuzuia uzalishaji na utengenezaji wa dawa za kulevya; na*

c) *Itaimarisha uwezo wa kupambana na uzalishaji na utengenezwaji wa dawa za kulevya.*

## 3.2 Usafirishaji, Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya husafirishwa na kusambazwa kupitia njia mbalimbali zikiwemo, kutumia kemikali; chakula cha kusindikwa; dawa tiba na vipodozi; kutoa taarifa za kughushi za mizigo inayosafirishwa; usafirishaji kupitia wanyama, magari binafsi; kupitia usafiri wa abiria; vifurushi vya posta; kumeza tumboni; vyombo vya majini kama mitumbwi, majahazi na meli pamoja na ndege zisizo na rubani. Serikali hufanya doria, upekuzi na ukamataji katika maeneo ya mipakani, viwanja vya ndege na bandari kwa lengo la kudhibiti uingizaji, usambazaji na usafirishaji wa dawa za kulevya. Hata hivyo, maendeleo ya teknolojia kama vile matangazo na biashara kupitia mitandao isiyo rasmi *(dark-web)* yamechangia usambazaji, ununuzi, uuzaji, utoaji, uhifadhi na umiliki wa dawa za kulevya kufanyika kwa hali ya usiri.

Nchi ya Tanzania hutumika kama njia ya kupitisha dawa za kulevya kwenda katika maeneo mengine kutokana na jiografia yake. Ili kudhibiti usambazaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, juhudi zaidi zikiwemo kuimarisha mifumo na mbinu za upekuzi pamoja na matumizi ya teknolojia ya kisasa vinahitajika ili kudhibiti mabadiliko ya mbinu za kuficha na kusafirisha dawa za kulevya na kemikali bashirifu. Aidha, msimamo wa nchi kisera unahitajika ili kuimarisha udhibiti katika njia kuu za usambazaji wa dawa za kulevya.

### 3.2.1 Lengo

Kudhibiti uingizwaji, usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini.

### 3.2.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

a) *Itaimarisha udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya inayofanyika kupitiateknolojia ya habari na mawasiliano;*

b) *Itajenga uwezo wa wadau katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya; na*

c) *Itaimarisha operesheni za kuzuia biashara ya dawa za kulevya.*

## 3.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Tanzania inakabiliwa na ongezeko la uhitaji na matumizi ya dawa za kulevya kama zilivyo nchi nyingine. Kundi linaloathirika zaidi ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 - 35. Sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa watu wanaojiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ni pamoja na tamaa ya kupata kipato kikubwa kwa haraka; kukosa malezi bora; jamii kutokuwa na elimu ya kutosha ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya; na msukumo wa makundi rika. Matumizi ya dawa za kulevya yanaathiri nguvu kazi ya Taifa na kusababisha mmomonyoko wa maadili na ustawi wa jamii kwa ujumla. Hivyo ni muhimu kuwa na mikakati ya kisera ili kulinda nguvu kazi ya Taifa kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

### 3.3.1 Lengo

Kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini.

### 3.3.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

a) *Itaimarisha utoaji wa elimu kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii;*

b) *Itaimarisha jitihada za kuzuia jamii kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya*; *na*

c) *Itaimarisha tafiti kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii.*

## 3.4 Uraibu na Magonjwa Yasiyoambukiza na Yanayoambukiza

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha madhara ya kiafya ikiwemo uraibu pamoja na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza yakiwemo magonjwa ya akili, saratani, magonjwa ya moyo, kiharusi, kifafa, magonjwa ya figo, VVU/UKIMWI na homa ya ini. Ongezeko hilo linatokana na dawa za kulevya kuathiri mifumo na viungo vya mwili. Matumizi ya dawa za kulevya yamechangia kupunguza nguvu kazi ya taifa, kuhatarisha afya za watumiaji na mara nyingine kusababisha vifo. Aidha, Serikali huingia gharama kubwa katika jitihada za kudhibiti matumizi, kutoa huduma za utengamao kwa watumiaji wa dawa ya kulevya.

Serikali kwa kushirikiana na wadau imechukua jitihada zinazolenga kupunguza madhara hayo zikiwemo kuhakikisha waraibu wa dawa za kulevya wanapata tiba ya uraibu na matatizo mengine ya kiafya, sambamba na kuwaunganisha

katika jamii na familia zao. Pia, huduma za utengemao pamoja na elimu ya upunguzaji madhara imeendelea kutolewa kwa waraibu wa dawa za kulevya. Huduma hizo zinatolewa kupitia vitengo vya afya ya akili katika hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa; nyumba za upataji nafuu (sober houses); vituo vinavyotoa tiba saidizi kwa waraibu wa *heroin* kwa kutumia dawa tiba ikiwemo *Methadone* na *Buprenorphine.* Vilevile, Serikali inatekeleza mpango wa kukabiliana na ugonjwa wa uraibu wa dawa za kulevya na magonjwa yasiyoambukiza yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Pamoja na jitihada hizo, waraibu wameendelea kuongezeka sambamba na kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya afya ya akili kutokana na matumizi ya dawa za kulevya zinazoathiri mifumo na viungo mbalimbali vya mwili. Aidha, uelewa wa jamii bado ni mdogo na huduma zinazotolewa hazikidhi ukubwa wa tatizo lililopo.

### 3.4.1 Lengo

Kupunguza uraibu wa dawa za kulevya, magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

### 3.4.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

*a) Itaimarisha huduma za tiba na utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya; na*
*b) Itaimarisha afua za lishe katika kukabiliana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya*

## 3.5 Uratibu wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka ambalo utekelezaji wake unahusisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Wadau hao ni pamoja na jamii yenyewe, Taasisi za Serikali, nchi jirani, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Dini, Taasisi zisizo za Serikali na Washirika wa Maendeleo. Lengo ni kuwa na mkakati wa pamoja wa kupambana na dawa za kulevya katika kuhakikisha dunia inakuwa salama dhidi ya dawa hizo.

Hata hivyo, hakuna mwongozo wa kisera unaotoa wajibu wa wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Hivyo ni muhimu udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya nchini kuhusisha vyombo vyote vya dola pamoja na wadau wote kwa kuzingatia mwongozo wa kisera na kisheria ili kufikia lengo la kuwa na jamii isiyojihusisha na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

### 3.5.1 Lengo

Kuimarisha uratibu wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini

### 3.5.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

*a) Itaimarisha mfumo wa uratibu wa pamoja wa wadau wanaojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya; na*

*b) Itaimarisha mfumo wa kisheria kwa ajili ya udhibiti na mapambano dhidi ya uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.*

## 3.6 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika Kukabiliana na Tatizo la Dawa za Kulevya

Tatizo la dawa za kulevya ni suala linalovuka mipaka na linalohusisha mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani. Dawa nyingi za kulevya zinazoingia nchini Tanzania zinatoka katika mataifa mengine na baadhi zinazalishwa hapa nchini. Hivyo, ushirikiano baina ya nchi na jumuiya za kikanda na kimataifa ni muhimu katika kukabiliana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Serikali imeridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali inayozielekeza nchi wanachama kuwa na sera mahsusi ya kudhibiti dawa za kulevya. Hata hivyo, pamoja na maelekezo hayo ya mikataba hiyo, bado nchi haina sera ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Ushirikiano wa kikanda na kimataifa unaziwezesha nchi wanachama kubadilishana uzoefu; kufanya operesheni za pamoja; mafunzo na kubadilishana teknolojia; na upatikanaji wa misaada mbalimbali. Hivyo, kuna umuhimu kuwa na sera ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ili kutekeleza kwa ufanisi Mikataba na Itifaki hiyo ya kikanda na kimataifa ili kuimarisha udhibiti wa uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

### 3.6.1 Lengo

Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya.

### 3.6.2 Matamko ya Sera

Serikali:

| |
|---|
| *Itaimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kudhibiti na kupambana na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.* |

## 3.7 Masuala Mtambuka

### 3.7.1 VVU na UKIMWI

Upo uhusiano wa karibu kati ya matumizi ya dawa za kulevya na VVU na UKIMWI kutokana na vitendo visivyo salama vya kuchangia vifaa vya kujidungia kwa wajidunga na kufanya ngono zisizo salama.

Serikali imeendelea kuimarisha utekelezaji wa afua za kudhibiti VVU na UKIMWI kwa kutoa elimu, kuboresha huduma za tiba kwa waraibu na ugawaji wa mabomba na sindano za kujidungia kwa wajidunga (*Needle and Syringes Programme* – NSP). Aidha, kumekuwa na ongezeko la maambukizi ya VVU na UKIMWI yanayochangiwa na matumizi ya dawa za kulevya kwa wajidunga.

#### 3.7.1.1 Lengo

Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

#### 3.7.1.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

a) *Itaimarisha afua za kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI kutokana na matumizi ya dawa za kulevya; na*
b) *Itakuza uelewa kuhusu athari za VVU na UKIMWI kwa watumiaji wa dawa za kulevya.*

## 3.8 Mazingira

Biashara na matumizi ya dawa za kulevya yana athari katika mazingira. Mapambano dhidi ya kilimo haramu cha mazao kama vile bangi na mimea ya mirungi huhusisha ukataji wa

miti na kusababisha kuenea kwa jangwa na ukosefu wa mvua; uchafuzi wa hewa; mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa ikolojia. Pia, uzalishaji wa dawa za kulevya na matumizi ya sindano husababisha uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji holela wa sindano za kujidungia zilizotumika pamoja na uzalishaji wa dawa za kulevya kwa kutumia kemikali bashirifu katika maabara bubu.

Serikali inadhibiti athari hizi kupitia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 4 ya mwaka 2004; kudhibiti uzalishaji wa mimea yenye asili ya dawa za kulevya na kuhamasisha kilimo mbadala katika mikoa inayolima mazao ya bangi na mirungi.

Hata hivyo, bado kuna changamoto za kukosekana kwa mwongozo wa kisera kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya zinazoathiri mazingira.

### 3.8.1 Lengo

Kuzuia na kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na uzalishaji na matumizi ya dawa za kulevya.

### 3.8.2 Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau:

a) *Itaimarisha ushirikiano na jamii ili kuzuia uharibifu wa mazingira kutokana na kilimo haramu, utengenezaji na uzalishaji wa dawa za kulevya; na*

b) *Itaimarisha utoaji wa elimu ya athari ya uzalishaji na matumizi ya dawa za kulevya katika mazingira.*

# SURA YA NNE

# MUUNDO WA KISHERIA

## 4.1 Mfumo wa Kisheria

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanaongozwa na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambayo imeweka mfumo na utaratibu wa kushughulikia dawa za kulevya nchini. Aidha, sheria imeanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yenye jukumu la kufafanua, kuhamasisha, kuratibu na kutekeleza afua zote zinazolenga kupambana na kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya unazingatia sheria nyingine kama ifuatavyo: Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177; Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219; Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443; Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256; Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61; Sheria ya Ulinzi wa Watoa Taarifa na Mashahidi, Sura ya 446; Sheria ya Ushirikiano Katika Masuala ya Jinai, Sura 254; Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura 423; na Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura ya 200.

Sheria nyingine ni pamoja na: Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306; Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; Sheria ya Afya ya Akili, Sura ya 98; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Takwimu, Sura ya 351; Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430; Sheria ya Miamala ya Kielekroniki, Sura ya 442; na Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368.

Kufuatia kutungwa kwa sera hii, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 itafanyiwa marekebisho ili kuwezesha utekelezaji wa sera. Aidha, baadhi ya sheria za kisekta zitafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia maelekezo na mahitaji ya sera.

# SURA YA TANO

# MUUNDO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.1 Muundo wa Kitaasisi

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya utaendelea kufanyika kwa kuzingatia muundo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yenye jukumu la kufafanua, kuhamasisha, kukamata watuhumiwa, kuchunguza na kupeleleza matukio mbalimbali ya dawa za kulevya. Mfumo huu utaendelea kuimarishwa ili uweze kukidhi azma ya Serikali ya kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Serikali, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Dini, na Jamii kwa ujumla. Mgawanyo wa majukumu na wajibu wa wadau katika kufanikisha utekelezaji wa afua za kudhibiti dawa za kulevya umefafanuliwa kama ifuatavyo:

### 5.1.1 Wizara yenye dhamana ya udhibiti wa Dawa za Kulevya

Wizara yenye dhamana ya udhibiti wa dawa za kulevya itakuwa na jukumu la msingi la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024.

### 5.1.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ina jukumu la kufafanua, kuhamasisha, kuratibu na kutekeleza hatua zote zinazoelekezwa katika udhibiti wa dawa za

kulevya. Katika kutekeleza jukumu hilo Mamlaka itasimamia utekelezaji wa Mkakati wa sera kwa kuzingatia mikakati mikuu minne (4) ambayo ni Kupunguza uingiaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya; Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya; Kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya; na Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa. Katika kuimarisha utekelezaji wa mikakati hiyo pamoja na mambo mengine Mamlaka itatekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

a) Kusimamia mkakati wa utekelezaji wa sera;

b) Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Dawa za Kulevya;

c) Kuandaa mkakati wa utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Sera;

d) Kuratibu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera kwa kushirikiana na wadau;

e) Kuandaa Taarifa kuhusu Hali ya Dawa za Kulevya Nchini; na

f) Kufanya tafiti kuhusu tatizo la dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na wadau.

**Wizara na Taasisi za Serikali**

### 5.1.2.1 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu utekelezaji wa programu za kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau;

b) Kuhakikisha masuala ya udhibiti wa dawa za kulevya yanajumuishwa kwenye Mipango na Bajeti za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

c) Kuweka miundombinu wezeshi ya utoaji wa huduma za afya ya akili katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

d) Kudhibiti maeneo ya vilevi kutumika kwa biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.2 Wizara yenye dhamana ya Kazi, Ajira na Vijana

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kutoa elimu kuhusu madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana; na

b) Kuwezesha vijana waliopata nafuu ya matumizi ya dawa za kulevya kupata ujuzi na kuwaunganisha na fursa za uwezeshaji kiuchumi na ajira.

#### 5.1.2.3 Wizara yenye dhamana ya Afya

Wizara itakuwa na jukumu la kuratibu masuala ya kitabibu ya kinga, matunzo na matibabu. Majukumu mahsusi yatakayotekelezwa ni pamoja na:

a) Kuhakikisha masuala ya dawa za kulevya yanajumuishwa katika Sera ya Afya;

b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya; na

c) Kufanya tafiti na kutoa miongozo na viwango vya utoaji wa huduma kwa waraibu.

#### 5.1.2.4 Wizara yenye dhamana ya Maliasili na Utalii

Wizara itakuwa na jukumu la kushiriki katika udhibiti wa uzalishaji wa mimea yenye asili ya dawa za kulevya katika hifadhi na misitu. Aidha, itashiriki katika kutoa elimu kuhusu udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa wadau wote wanaohusika na utalii.

#### 5.1.2.5 Wizara yenye Dhamana na Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Makundi Maalum

Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na makundi maalum itakuwa na wajibu wa kutekeleza sera kwa kujumuisha malengo ya sera kwenye mipango yake. Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:

a) Kutoa miongozo itakayowezesha kukuza maadili katika jamii ili kufikia malengo ya kuwa na jamii isiyojihusisha na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya;

b) Kuhimiza malezi bora katika ngazi ya jamii ili kuwa na familiabora zenye kuzingatia maadili ya Mtanzania;

c) Kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waathirika wa dawa za kulevya; na

d) Kufanya ufuatiliaji kwa jamii iliyoathirika na matumizi ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.6 Wizara yenye dhamana ya Elimu

Wizara yenye dhamana na elimu itakuwa na majukumu yafuatayo:-

a) Kuandaa mitaala itakayozingatia ufundishwaji wa afua za dawa za kulevya katika ngazi zote za elimu ili kuandaa wanafunzi kuwa na uelewa kuhusu madhara ya dawa za kulevya;

b) Kutoa elimu ya athari ya dawa za kulevya katika ngazi zote za elimu; na

c) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya dawa za kulevya.

### 5.1.2.7 Wizara yenye dhamana ya Fedha

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya sera pamoja na mkakati wake;

b) Kusimamia na kuhakikisha fedha zilizotolewa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa;

c) Kudhibiti mifumo ya fedha isiyo rasmi ikiwemo matumizi ya fedha za kidijitali katika kutekeleza uhalifu; na

d) Kuimarisha udhibiti katika maeneo ya forodha na usafirishaji wa vifurushi.

### 5.1.2.8 Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi

Wizara itakuwa na jukumu la kuimarisha mifumo ya usafiri, usafirishaji na ukaguzi wa abiria, mizigo pamoja na bidhaa zinazoingizwa na kutoka nchini ili kudhibiti usafirishaji wa dawa za kulevya.

#### 5.1.2.9 Wizara yenye dhamana ya Kilimo

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti kilimo cha mimea yenye asili ya dawa za kulevya. Aidha, itakuwa na jukumu la kufanya tafiti za mazao mbadala kwenye maeneo yanayojihusisha na kilimo cha mimea yenye asili ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.10 Wizara yenye dhamana na Mawasiliano

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:

a) Kuweka mifumo ya ufuatiliaji wa shughuli za kutuma na kupokea vifurushi;

b) Kuratibu na kusimamia mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kudhibiti uhalifu wa kimtandao; na

c) Kuratibu vyombo vya habari katika utoaji wa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.11 Wizara yenye dhamana ya Sheria

Wizara hii itajumuisha masuala ya udhibiti wa dawa za kulevya kwenye mfumo wa usimamizi wa haki na haki jinai nchini. Aidha, itaratibu masuala ya kisheria kuhusu urejeshwaji wa wahalifu wanaohusika na mashauri ya dawa za kulevya kwenye nchi wanazotuhumiwa kutenda uhalifu ambazo Tanzania ina makubaliano na nchi hizo.

#### 5.1.2.12 Wizara yenye dhamana ya Viwanda na Biashara

Wizara hii itakuwa na jukumu la kuimarisha udhibiti wa uzalishaji na biashara ya bidhaa zenye asili ya kulevya na bidhaa zinazochanganywa na dawa za kulevya.

#### 5.1.2.13 Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Wizara hii itaratibu masuala ya dawa za kulevya yenye kuhitaji mwitikio wa kikanda na kimataifa.

#### 5.1.2.14 Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Wizara hii itakuwa na jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao dhidi ya athari za uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.15 Wizara yenye dhamana ya Madini

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwenye maeneo ya migodi ya madini. Aidha, wizara itakuwa na jukumu la kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu zinazotumika migodini.

#### 5.1.2.16 Wizara yenye dhamana ya Nishati

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti uchepushwaji wa mafuta, gesi na nishati nyingine zisitumike kutengeneza dawa za kulevya.

#### 5.1.2.17 Wizara yenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti biashara, matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya kwa wadau wa mifugo na uvuvi. Aidha, itakuwa na jukumu la kudhibiti uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya zinazotumika kwenye mifugo.

#### 5.1.2.18 Wizara yenye dhamana ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti biashara, matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya kwa wadau wa Michezo, Utamaduni na Sanaa. Aidha, Wizara itakuwa na jukumu la kukuza maadili ya Taifa ili kuepusha jamii kujiingiza katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.19 Wizara yenye dhamana ya Mipango na Uwekezaji

Wizara hii itakuwa na jukumu la kuhakikisha madhara ya dawa za kulevya yanazingatiwa kwenye mipango mbalimbali ya Taifa.

#### 5.1.2.20 Wizara yenye dhamana ya Mazingira

Wizara hii itakuwa na jukumu la kuratibu utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya uzalishaji na matumizi ya dawa za kulevya kwenye mazingira.

#### 5.1.2.21 Wizara yenye dhamana ya Maji

Wizara hii itakuwa na jukumu la kudhibiti na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya uzalishaji wa dawa za kulevya kwenye vyanzo vya maji na maeneo oevu.

#### 5.1.2.22 Wizara yenye dhamana ya Ardhi na Makazi

Wizara hii itakuwa na jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya ardhi ili kuepusha jamii kujihusisha na uzalishaji wa dawa za kulevya.

#### 5.1.2.23 Wizara yenye dhamana ya Ulinzi

Wizara hii itakuwa na jukumu la kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi kavu na majini dhidi ya uingizwaji wa dawa za kulevya.

#### 5.1.2.24 Wizara yenye dhamana ya Utumishi

Wizara hii itakuwa na jukumu la kuratibu utoaji elimu ya maadili ikiwemo madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa watumishi wa umma.

#### 5.1.2.25 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Ofisi hii itawezesha utungwaji wa sheria mpya na marekebisho ya sheria mbalimbali za kisekta ili kuwezesha utekelezaji wa sera.

#### 5.1.2.26 Vyombo vya Ulinzi na Usalama

Vyombo vya ulinzi na usalama vitashirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Aidha, vyombo hivyo vitakuwa na jukumu la kuimarisha mifumo ya kudhibiti uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, vyombo hivyo vitashiriki na kuwezesha upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi mbalimbali kwa ajili ya operesheni za udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

#### 5.1.2.27 Taasisi yenye dhamana ya Dawa na Vifaa Tiba

Taasisi yenye dhamana ya dawa na vifaa tiba itakuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia biashara na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kuathiri upatikanaji wake kwa matumizi halali.

#### 5.1.2.28 Taasisi yenye dhamana ya Usimamizi wa Kemikali

Taasisi yenye dhamana ya kemikali itakuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia biashara na matumizi ya kemikali bashirifu bila kuathiri upatikanaji wake kwa matumizi halali.

#### 5.1.2.29 Tawala za Mikoa

Tawala za Mikoa zitakuwa na jukumu la kudhibiti uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### 5.1.2.30 Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji

Halmashauri ni vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sera mbalimbali za kisekta. Kwa msingi huu, Halmashauri zitashiriki katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kuimarisha udhibiti wa uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi za msingi za Serikali za Mitaa;

b) Kujumuisha afua za dawa za kulevya katika mipango ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

c) Kutunga na kutekeleza Sheria Ndogo za kukabiliana na dawa za kulevya.

#### 5.1.2.31 Ngazi ya Kata

Majukumu yafuatayo yatatekelezwa katika ngazi ya Kata:

a) Kuratibu na kusimamia udhibiti wa uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya Kata; na

b) Kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo za kukabiliana na dawa za kulevya.

### 5.1.2.32 Ngazi ya Kijiji/Mtaa

Ngazi ya Kijiji/Mtaa ni ngazi ya msingi ya utawala ambayo inagusa maisha ya watu wote nchini. Kijiji/Mtaa ni kitovu cha utekelezaji wa afua za dawa za kulevya zinazolenga jamii. Kijiji/Mtaa kitakuwa na jukumu la kusimamia afua za dawa za kulevya katika ngazi ya Kijiji/Mtaa na Kitongoji kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

a) Kuhamasisha na kuhimiza jamii kutojihusisha na uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya;

b) Kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo za kukabiliana na dawa za kulevya katika ngazi ya Kijiji/Mtaa; na

c) Kuimarisha mfumo wa utoaji taarifa kuhusu matukio yanayohusisha dawa za kulevya.

### 5.1.2.33 Ngazi ya Kaya

Ngazi ya Kaya inawajibika kutekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kutoa malezi bora kwa familia kwa ajili ya kujenga maadili, uzalendo na ustawi wa jamii; na

b) Kutoa elimu kuhusu madhara ya uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa kaya.

### 5.1.2.34 Sekta Binafsi

Sekta binafsi ndiyo mhimili wa ukuaji wa uchumi wa nchi kutokana na fursa za ajira. Sekta binafsi itatekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kukuza fursa za uwekezaji na kuongeza fursa za ajira zitakazosaidia jamii kujiepusha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya;

b) Kuchangia juhudi za Serikali katika udhibiti wa uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya; na

c) Kushiriki kikamilifu kwa kutoa taarifa katika udhibiti wa dawa za kulevya, kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

### 5.1.2.35 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs)

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatashirikiana na Serikali na Wadau wengine katika kupanga na kuweka vipaumbele vya afua za dawa za kulevya, ikijumuisha matibabu, kupunguza athari/ madhara na masuala mtambuka; kutekeleza programu za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu afua za dawa za kulevya nchini na kutafuta rasilimali za kusaidia utekelezaji wa afua za kudhibiti dawa za kulevya.

### 5.1.2.36 Taasisi za Kidini

Mashirika/Taasisi za kidini nchini zitashiriki katika kuhamasisha maadili ya jamii kwa ajili ya kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Taasisi hizi zitahusika katika kutoa mafundisho ya kiroho kwa makundi yote kwenye jamii ambayo yatasaidia kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya.

### 5.1.2.37 Wadau wa Maendeleo

Wadau wa Maendeleo watashirikiana na Serikali katika kuwezesha mkakati wa utafutajiwa rasilimali za utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 katika ngazi mbalimbali za Serikali. Aidha, wadau hawa watasaidia katika kujenga uwezo wa mfumo wa nchi wa kukabiliana na dawa za kulevya.

### 5.1.2.38 Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vitashiriki katika kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya sera pamoja na kuelimisha jamii kuhusu athari za uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

## 5.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na dawa za Kulevya ni mchakato endelevu. Wizara yenye dhamana ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera kwa kushirikisha wadau. Taarifa itaandaliwa kwa kuzingatia viashiria vya kupima mafanikio/malengo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024. Jukumu la kuandaa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini litakuwa la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Wizara yenye dhamana ya kuratibu udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na wadau wengine wa ngazi mbalimbali za utekelezaji.

Ili kuwa na ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itaandaa na kuboresha mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuongeza ufanisi. Wizara yenye dhamana ya kuratibu udhibiti wa Dawa za Kulevya itakuwa kiungo cha uratibu huo na sekta nyingine ikiwemo ushiriki wa sekta binafsi. Mfumo wa ukusanyaji taarifa/takwimu utaanzishwa ndani ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na tathmini ya mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa sera itafanyika na matokeo ya tathmini yatatumika kuboresha sera, mkakati na mipango mbalimbali ya kudhibiti dawa za kulevya. Tathmini ya utekelezaji wa sera itafanyika kila mwaka na taarifa itajadiliwa katika mikutano ya wadau.

## 5.3 Hitimisho

Madhumuni ya Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024 ni kutoa mwongozo wa jumla wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini kwa kuzingatia mipango na mikakati ya kitaifa pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa. Udhibiti wa dawa za kulevya umejikita katika kuleta usalama na amani ya nchi; na

kuwa na jamii isiyojihusisha na uzalishaji biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Sera imezingatia pia mabadiliko yaliyotokea duniani katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na kimazingira. Aidha, Sera imezingatia masuala mtambuka ya VVU na UKIMWI na utunzaji wa mazingira.